OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

**SHULE YA SEKONDARI KISAKA,**
**S.L.P 08,**
**MUGUMU-SERENGETI.**
**………../………/2020**

**Kumb. Na.KSS/JI – 2020/18**
Jina la Mwanafunzi ______________________
S/Msingi____________________
S.L.P ______________________
______________________

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISAKA

WILAYA YA SERENGETI MKOA WA MARA CHAGUO LA KWANZA-2020

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha I katika shule hii mwaka **2021.** Shule ya Sekondari **KISAKA** ipo umbali wa Km **60** kaskazini mwa Halmashauri ya Wilaya ya **Serengeti barabara ya Tarime kupitia Nyamongo**.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021.** Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe **04/01/2021.**

- UNAPASWA KUWAHI ILI USIACHWE NA WENZAKO KWENYE MASOMO YA AWALI .

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

a) **Sare za Shule**

**2.1.1 Za Darasani**

a) **WAVULANA**

Sare za Shule hii kwa wavulana ni;-

- Shati Nyeupe 02 za mikono mifupi
- Suruali za bluu bahari 02-kitambaa kizito-***YENYE MIFUKO MITATU (HATURUHUSU MODAL)***
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba.
- Tai ndefu ya bluu bahari
- Soksi nyeusi pair 02

b) **WASICHANA**

Sare za Shule hii kwa wasichana ni;-

- Shati Nyeupe 02 za mikono mifupi.
- Sketi za bluu bahari 02 (mshono wa marinda-kitambaa kizito)
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba
- Rangi ya Hijab ifanane na sare za Shule (kwa Waislam)
- Tai ndefu ya bluu bahari
- Soksi nyeupe pair mbili

#### 2.1.2 MICHEZO

**a) WAVULANA**

- Sare za Shule hii kwa Wavulana ni T-Shirt nyekundu, Bukta ya rangi ya bluu na viatu vya michezo.

**b) WASICHANA**

- Sare za Shule hii kwa Wasichana ni T-Shirt njano, Trakisuti ya rangi ya bluu na viatu vya michezo..

### 2.2 MAHITAJI YA DARASANI

a. **DAFTARI ZA KUTOSHA-(KAUNTA BOOK 09 KWAAJILI YA MASOMO YA DARASANI NA DAFTARI NDOGO 09 KWAAJILI YA KOZI YA KIINGEREZA) KALAMU NA MKEBE WA HESABU.**

b. **FEDHA YA TAALUMA KWAAJILI YA WALIMU WA MUDA KWA MUJIBU WA MAKUBALIANO YA KIKAO CHA WAZAZI– TSH 20,000/= (KWA MWAKA), 10,000/= (KWA MUHULA) AU 2000/= KWA MWEZI**

c. **KAMUSI YA KIINGEREZA/KISWHILI –OXFORD DICTIONARY**

d. **RIMU YA KARATASI KWA MAKUBALIANO NA WAZAZI.(A4)**

e. **KITI NA MEZA VYENYE CHUMA KWA CHINI ILI KUZUIA KUCHIMBA SAKAFU.**

**SHULE INA UPUNGUFU WA VITI NA MEZA, VILIVYOPO HAVIWATOSHI.HIVYO KILA MZAZI AHAKIKISHE MWANAE ANAPATA KITI NA MEZA, WAKATI SERIKALI IKIJIPANGA KUTATUA HILI.**

### 2.3 Chakula cha Wanafunzi (kwa muhula)

#### 2.3.1 Wa Kutwa

- **Mahindi Kg 30 , Maharage Kg 15,**
- **Fedha taslim 2000/= kwa ajili kusaga kwa muhula mmoja**
- **Fedha ya mpishi(lazima) sh.3000 kwa muhula mmoja**

#### 2.3.2 Wa Hostel

- **Mahindi Kg 60, Maharage Kg 30(kwa muhula)**
- **Fedha Taslim 40,000/= kwa muhula**

## 2.4 Mahitaji ya HOSTEL (WASICHANA)

*MAHITAJI MUHIMU KWA WANAFUNZI WANAOKAA HOSTEL MWAKA 2021*

1. *CHAKULA KWA MUHULA MMOJA.*
   - *1.1. Mahindi – kg 60*
   - *1.2. Mchele - kg 06*
   - *1.3. Maharage- kg 30*
   - *1.4. Mafuta ya kupikia- Lita 04*
   - *1.5. Chumvi- kg 02*
2. *HUDUMA.*
   - *2.1. Pesa kwa ajili ya; kusaga, Kulipa wapishi na ukarabati wa vitanda vya Hoste,umemel jumla Tsh.40,000/=*
   - *2.2. Taa inayotumia mionzi ya jua kwa ajili ya dharura kujisomea.pindi umeme ukikatika*
3. *MATANDIKO.*
   - *3.1 . Godoro 2.5x6 (Aje nalo).*
   - *3.2.Mashuka 2 (Blue 1, pinki 1 ).*
   - *3.3 Chandarua 1.*
   - *3.5. Mto wenye foronya 1 ila sio lazima.*
4. *VIFAA VYA USAFI BINAFSI.*
   - *4.1. Kandambili pair 1.*
   - *4.2. Taulo.*
   - *4.3. Dawa ya meno.*
   - *4.4. Sabuni ya kufulia.*
   - *4.5. Mafuta ya kujipaka ya mgando.*
   - *4.6.Ndoo ya plastiki.*
   - *4.7. Beseni la kufulia*
5. *VYOMBO VYA CHAKULA.*
   - *5.1. Sahani yenye partition ya alluminium*
   - *5.2. kikombe.*
6. *SARE MAALUMU ZA HOSTEL.*
   - *6.1. T-shirt 02 za njano*
   - *6.2. Kanga vipande 02.*
   - *6.3. Truck Suit ya rangi ya bluu*

*NB:*

***-Kama mwanafunzi ana matatizo yanayomzuia kula chakula kilichotajwa hapo juu, hataruhusiwa kuishi hosteli kwa sababu hakutakuwepo na chakula mbadala.***

***'Hostel ni mazingira mazuri kwa mwenye jitihada za kutaka ufaulu'***

7. *TARATIBU ZA KUISHI HOSTEL*

*-Sheria za kuishi hostel ni zilezile anazotakiwa mwanafunzi kuzitii wakati wote awapo shuleni, nyumbani, njiani/barabarani aendapo na atokapo shuleni. Baadhi ya sheria hizi ni kama ifuatavyo;*

- *7.1. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki simu.*
- *7.2. Mavazi yasiyo sare ya shule au Hosteli hayatakiwi.*
- *7.3. Ni marufuku kulala nje ya Hosteli bila kibali maalumu.*
- *7.4. Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa.*
- *7.5 Kubaki ndani ya jengo la Hosteli wakati wa masomo, prepo(maandalio ya jioni) au matukio mbalimbali ni kosa na utaadhibiwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.*
- *7.6. Kila mwanafunzi wa Hosteli anatakiwa kutii ratiba ya shule pamoja na ile ya Hosteli.*
- *7.7 Mwanafunzi hatapokelewa kama hana mahitaji yote yanayohitajika Hosteli.*
- *7.8 Mwanafunzi awapo Hosteli hataruhusiwa kwenda nje ya eneo la shule kwa sababu yoyote ile, isipokuwa kwa dharura ya ugonjwa au kushiriki ibada chini ya uangalizi wa mwalimu.*

**3.0 Sheria na Kanuni za Shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya elimu Na. 23 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aitha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na OFISI YA RAIS – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya muhimu yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
g) Kuvaa sare ya shule wakati worte unapotakiwa,
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za Umma.

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi;**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shulw mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***KUMBUKA TAREHE YA KURIPOTI NA TAREHE YA JARIBIO LA UTHIBITISHAJI.***

**KARIBU SANA**

..........................................

MBOGGO J,B

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KISAKA
S.L.P. 08, MUGUMU
SERENGETI

KIAMBATANISHO A(ijazwe na daktari)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

KISAKA SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 08, MUGUMU

---

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF A STUDENT SELECTED TO JOIN FORM ONE (I) -2021 (YEAR)

Medical Officer;

______________________________

______________________________

______________________________

Name of a Pupil ____________________________________________

Please examine the above mentioned as to his/her fitness for Secondary School education according to the following items below;

| S/No. | ITEM | CONDITION | REMARKS |
|---|---|---|---|
| 1. | Mental Condition | | |
| 2. | Sight | | |
| 3. | Hearing | | |
| 4. | Chest TB | | |
| 5. | Urine | | |
| 6. | Stool | | |
| 7. | Nose | | |
| 8. | Blood Pressure | | |
| 9. | Pregnancy | | |
| 10 | Blood Group | | |
| 11. | HB | | |
| 12 | Others | | |

Any other Physical disability not listed that may affect his/her studies ________________

________________________________________________________________

________________________________________________

Signed: ______________________________

MEDICAL OFFICER & OFFICIAL STAMP

NYONGEZA B(ijazwe na mwanafunzi)

SHULE YA SEKONDARI KISAKA,
S.L.P 08,
MUGUMU.

HATI YA KUKUBALI (MWANAFUNZI)

Mimi ______________________________ wa Shule ya Msingi ____________________ Nakubali/Sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na Kidato cha Kwanza kwenye Shule hii. Naahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa uwezo wangu, nitafuata Sheria na Kanuni za shule.

NITASOMA KWA BIDII NA NIDHAMU NZURI WAKATI WOTE NITAKAPOKUWA MWANAFUNZI WA SHULE HII.

Sahihi: ______________________________ Tarehe: ____________________

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ______________________________ Tarehe: ____________________

*FUTA LISILOHUSIKA

******************************************************************************************

NYONGEZA C(ijazwe na mzazi au mlezi)

SHULE YA SEKONDARI KISAKA,
S.L.P 08,
MUGUMU.

HATI YA KUKUBALI NA KUTEKELEZA WAJIBU KAMA (MZAZI/ MLEZI).

Mimi(majinamatatu)______________________________Mzazi/mlezi wa mwanafunzi______________________________ambaye ni(uhusiano)____________________ nahidi ya kwamba (Nitakuwa/sitakuwa) mstari wa mbele kushirikiana na uongozi wa Shule ya Sekondari KISAKA katika kumlea mwanafunzi tajwa hapo juu na kumhudumia mahitaji mbalimbali yaliyokubalika katika kipindi chote cha kusoma kwake shuleni.Pia nitafatilia mwenendo wa mwanafunzi anapokuwa Shuleni au nje ya Maeneo ya shule.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ______________________________ Tarehe: ____________________

**Unapoishi(kijiji/mtaa)**______________**kata**__________**wilaya**______________

**Simu**____________________